
# THE SACRED NAME BROADCASTER

## Mtangazaji wa Jina Takatifu



5/2026

a publication of ***Assemblies of Yahweh***

THE SACRED NAME BROADCASTER

*An **Assemblies of Yahweh** publication.*
***Assemblies of Yahweh**, **The Narrow Way Newsletter**, **The Sacred Name Broadcaster**, **The Sacred Name Broadcast**, **The Sacred Scriptures**, **The Sacred Name Telecast**, and **WMLK Radio** are Service Marks and Trademarks of Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507*

***May 2026***
***Volume LVIII, Number 2***

# YALIYOMO



Page 1

1 ***Jinsi ya Kusoma Biblia***
*Njia moja nzuri zaidi ya kuthibitisha ukweli wa Maandiko ni kwa kuonyesha utimilifu wa unabii wa Biblia. Upatano wa Biblia kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo utafikiwa kwa kujifunza Biblia kwa bidii. Kusoma Maandiko mara kwa mara ni hatua muhimu ya kuelewa Maandiko na kujifunza Biblia vizuri. "Kila andiko, lenye punzi ya Yahweh, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Yahweh awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema." (2 Timotheo 3:16-17).*

8 ***Zawadi yetu kwa Ulimwengu: Maarifa ya Neno la Uzima***
*Ujumbe wa Ukweli utahubiriwa hadi miisho ya dunia kabla tu ya Yahshua Messiah kurudi. Ujumbe wa Ukweli unawahimiza watu wote kukumbuka Sheria ya Musa-amri za Mwenye-nguvu Yahweh. Je, utakubali mafundisho haya safi ya Neno la Yahweh na kujitayarisha kwa Ujio wa Pili wa Yahshua Messiah?*

11 ***Alama ya Yahweh dhidi ya Alama ya Mnyama, Sehemu ya 1***
*Kwa hakika kuna alama kwa WATU WA YAHWEH. Kinyume na chapa ya Yahweh, hata hivyo, itakuwa alama ya pekee ya Mnyama. Hizi ni alama mbili ambazo zimetajwa katika Maandiko. Wenye haki watatiwa alama ya Yahweh. Waovu pia watatiwa alama vilevile.*



Page 6


Page 10

## Jalada Letu

***"Wapandao kwa machozi watavuna kwa furaha. Ingawa mtu anakwenda zake akilia, azichukuapo mbegu za kupanda. Hakika atarudi kwa kelele za furaha, aichukuapo miganda yake."** (Zaburi 126:5-6).*

*Kupanda mbegu ya thamani ya Kweli kunahitaji Imani kuu, tukijua kwamba ni Yahweh atoaye mavuno, kama vile Mtume Paulo alivyoonyesha, **"Mimi nilipanda," alisema, "Apolo akatia maji, lakini Yahweh ndiye aliyekuza."** (1 Wakorintho 3:6).*




*Mzee Jacob O Meyer (OBM) alichukua hatua kubwa ya imani alipoanza kuchapisha The Sacred Name Broadcaster miaka 58 iliyopita. Mamilioni ya majarida yametumwa tangu wakati huo, katika nchi zaidi ya 100 ulimwenguni pote. **"Apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu."** (2 Wakorintho 9:6b).*

*Jalada letu la mwezi huu linaonyesha shamba lililoiva la ngano, na kutukumbusha kuwazia mavuno yanayokaribia. **"Hamsemi ninyi, bado miezi minne, ndipo yaja mavuno? Tazama, mimi nawaambieni, inueni macho yenu myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno."** (Yohana 4:35).*

*Je, katika shamba hili la ulimwengu, utazaa mavuno mengi au kuruhusu Adui akuibie mavuno? **"Na zilizoanguka penye miiba ni wale waliosikia, na katika kuenenda kwao husongwa na shughuli na mali, na anasa za maisha haya, wasiivishe lolote. Na zile penye udongo mzuri, ndio wale ambao kwa unyofu na wema wa mioyo yao hulishika neno, na kulishika; kisha huzaa matunda kwa kuvumilia."** (Luka 8:14-15).*

Mtangazaji wa Jina Takatifu huchapishwa kila mwezi na Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507. Uandikishaji wako umelipwa na watendakazi wenza wenye hiari wa huduma hii ambao wanajali kwamba ujumbe huu wa wokovu unapaswa kutolewa bila malipo kwa ulimwengu wote kama shahidi kabla ya Ujio wa Pili wa Yahshua Masihi. Ingawa hakuna malipo yoyote yatakayotozwa kwenye chapisho hili, MICHANGO (yote inakatwa kodi) inakubaliwa kwa shukrani ili kusaidia kulipia gharama. Tunatumahi kuwa utashiriki katika kufanya habari hii ipatikane kwa wengine.

Nukuu zote katika The Sacred Name Broadcaster zimetolewa kwa The Sacred Scriptures, Bethel Edition, 1981, Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507, isipokuwa ikitangazwa vingenevyo. Tafsiri zote za Biblia humu, zimesahihishwa ziwe thabiti na maandishi yaliyo ya awali zaidi yanayopatikana. Nakala za The Sacred Scriptures, Bethl Edition, zinapatikana. Kwa ujumbe jinsi ya kununua kopi yako, andika kwa Assemblies of Yahweh.

© Hakimiliki 2026 Assemblies of Yahweh. Haki zote zimehifadhiwa.
Malipo ya posta ya mara kwa mara huko Reading, PA 19612 (ISSN 879320). Simu (717) 933-4518. POSTA: Tuma fomu 3579 kwa Assemblies of Yahweh, SLP C, Bethel, PA 19507.

***Mwanzilishi na Mwandishi:** Mzee Jacob O. Meyer*

# Jinsi ya Kusoma Biblia




***na Mzee Jacob O. Meyer***

Kwa ukawaida unaoongezeka, ninapokea maswali kuhusu njia bora zaidi ya kujifunza Biblia kutoka kwa watu ambao wamejitolea maisha yao kwa Mwenye-nguvu. Wengi wanaosoma **The Sacred Name Broadcaster** wamekuwa na wasiwasi kuhusu matatizo yanayoongezeka ya nyakati zetu za taabu. Ni dhahiri kwa wale walio makini na hali ya dunia kwamba mgogoro mkubwa unajengeka. Utafutaji usio na matunda katika sehemu za kilimwengu wa majibu ya matatizo ya maisha hatimaye umewaongoza wengi wa watafutaji hawa wa Kweli katika kutafakari kwa uzito ujumbe wa Biblia.

Moja ya njia nzuri zaidi kuthibitisha Ukweli wa Maandiko ni kwa kuonyesha utimizo wa unabii wa Biblia. Mtu anapojifunza Biblia kwa nia ya kuthibitisha ukweli wake, ni lazima akabiliane na unabii mwingi uliotimizwa unaopatikana katika Maandiko yaliyoongozwa.

Upatanisho wa Biblia kutoka Mwanzo hadi Ufunuo hutuongoza kwenye hitimisho kwamba Kusanyiko la Kitume la Agano Jipya lilipata msingi thabiti wa Imani yao katika Messiah ndani ya unabii wa Agano la Kale.

Mtume Petro alionyesha hili kwa ufanisi kabisa aliposema. ***"Kwa hiyo ndugu, kufanye imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe. Maana***




***hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika Ufalme wa milele wa Mfalme wetu, Mwokozi wetu Yahshua Messiah. Kwa hiyo nitakua tayari kuwakumbusha hayo siku zote, ijapokua mnajua na kuthibitishwa katika kweli mliyo nayo."*** (2 Petro 1:10-12).

***"Maana alipata kwa Yahweh aliye Baba heshima na utukufu, hapo alipoletewa sauti iliyotoka katika utukufu mkuu, huyu ni mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye. Na sauti hiyo sisi tuliisikia ikitoka mbinguni tulipokuwa pamoja naye katika mlima ule mtakatifu. Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'aayo mahali penye giza, mnafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu."*** (2 Petro 1:17-19).

Petro alituachia rekodi ya imani yake katika unabii wa Biblia, akiuita hakika (hakika na kamili). Alikuwa na mawasiliano ya kibinafsi na Messiah. Mawasiliano haya ya kibinafsi yalitoa uthibitisho ulio hai wa usahihi wa Maandiko yaliyoongozwa, kwa kuwa Yahshua aliye Messiah alikuwa hapo awali amekuwa na jukumu kubwa katika kuyatunga. Baada ya kufufuka Kwake Yahshua aliwafungulia wanafunzi wake ufahamu wa unabii wa Biblia kumhusu. (Luka 24:44-46).

Mahali penye mantiki pa kuanzia kusomo kwako kwa Biblia lazima pawe ni kijithibitishia mwenyewe uvuvio wa uandishi wake. Mtume Paulo, akimwandikia mhubiri mwanafunzi Timotheo, alisema, ***"Kila andiko, lenye pumzi ya Yahweh, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki: ili mtu wa Yahweh awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."*** (2 Timotheo 3:16-17) (Tambua kwamba kitenzi cha kwanza *ni* hakionekani katika maandishi ya awali; kwa hiyo istilahi iliyotolewa, *kwa pumzi ya Yahweh* hurekebisha neno maandiko likisimama katika nafasi ya kuashiria.) Tafsiri halisi ya neno lililotumika katika **King James** lililopulizwa na Yahweh, katika maandishi ya Kigiriki kwa kweli humaanisha, *iliyopuliziwa na Yahweh*, au *aliyopulizia Yahweh*.

Paulo alikuwa akielezea kwamba yote ya Maandiko ya kibiblia yaliyoandikwa zamani na manabii wa Agano la Kale yalikuwa yamepuliziwa kwa njia isiyo ya kawaida, au kuvuviwa (yaliyofunuliwa), na Roho wa Baba wa Mbinguni Aliye Juu Sana, Yahweh. Mwana-habari njema wa Agano Jipya aliamini kwamba Yahshua alikuwa ametimiza unabii wa kibiblia hadi kwa herufi halisi (hata kwa tarehe ya kuonekana kwake) iliyoandikwa kumhusu Yeye maelfu ya miaka kabla ya kufanya kuonekana Kwake. Walikuwa wakitumia unabii huu wa kimaandiko kuthibitisha ukweli wa dai la kimessiah.

Kwa hiyo, ni lazima tuhitimishe kwamba maandishi ya wanahabari njema Mathayo, Marko, Luka, na Yohana yana rekodi ili-

yoongozwa na Roho Mtakatifu ya Messiah ambaye alitimiza unabii wa Agano la Kale. Vivyo hivyo, lazima tutambue maandishi ya Mtume Paulo kuwa yamevuviwa kama vile Maandiko matakatifu mengine yote, kwa sababu ya yale ambayo Petro alisema kuyahusu. Tambua kutoka 2 Petro 3:15-16. Kwamba Petro aliamini kabisa kwamba maandishi ya Paulo yalikuwa yaliyovuviwa. ***"Nanyi uhesabuni uvumilivu wa Mwokozi wetu kuwa ni wokovu, kama vile na ndugu yetu mpenzi Paulo alivyowaandikia kwa hekima aliyopewa. Vile vile kama katika nyaraka zake zote pia, akitoa humo habari za mambo hayo. Katika nyaraka hizi yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo, na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa, kama vile wayapotoavyo na maandiko mengine, kwa uvunjifu wao wenyewe."*** (2 Petro 3:15-16). **New International Version** [N.I.V.]).

Mwishoni mwa Biblia ni kitabu cha Ufunuo. Utangulizi wake unatuongoza kuamini kwamba kitabu hiki, ambacho kinahitimisha maandishi ya Biblia, lazima pia kijumuishwe katika kanuni iliyovuviwa.

Mwishoni mwa Ufunuo linapatikana onyo kali dhidi ya kuchezea maandishi yake na, kwa kuongezea, yale ya Biblia nzima. ***"Namwonya kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, mtu yeyote akiyaongeza, Elohim atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Naye mtu yeyote akiondoa lolote katika kitabu maneno ya unabii wa kitabu hiki, Elohim atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki."*** (Ufunuo 22:18-19, [**N.I.V**]). Onyo hili linayarudia yale tunapata katika Kumbukumbu la Torati 4:2, 12:32, na Mithali 30:6.

Baada ya kujihakikishia mwenyewe uvuvio wa Biblia, na kuamua kusoma yaliyomo kwa makini, inakuwa muhimu kusafisha akili yako kutokana na mafundisho yote yaliyotangulia ili kwamba unaweza kuelewa kikamilifu kile ambacho Roho Mtakatifu unakataa kuwasilisha. "Ni vigumu zaidi kujisahaulisha makosa kuliko kujifunza kweli," ni msemo sahihi

Yahshua aliye Messiah alijua na kufunza kwamba mila na desturi za mataifa (watu wa mataifa) zilikuwa zinazopingana na mafundisho ya Biblia. Geukia kwa Mathayo 6:30-33 kwa uthibitisho. ***"Basi, ikiwa Elohim huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo, na kesho hutupwa kwenye tanuri, je, hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba? Msisumbuke, basi, mkisema tule nini? Au tunywe nini? Au tuvalie nini? Kwa maana hayo yote Mataifa huyafuata; kwa sababu Baba yenu wa Mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa."***

Kumbukumbu la wakati ambapo mhariri na mkewe walianza kujifunza kwa bidii Maandiko yaliyoongozwa labaki wazi kabisa. Tulikabiliana kikamilifu na Maandiko mbalimbali ya Agano Jipya yaliyoandikwa na Mtume Paulo, ambayo makanisa ya kilimwengu yananukuu kuthibitisha kwamba sheria ya Yahweh si ya kufuatwa tena katika enzi hii ya Agano Jipya. Tulijiuliza, "Je, hazikupingana na yale ambayo tayari yameandikwa katika Agano la Kale?" Ni vipi tungeyaelewa?

Tulijua kwamba dhambi, kwa ufafanuzi, ni uvunjaji wa sheria za Yahweh (1 Yohana 3:4). Pia tulijua kwamba Waabudu wa kweli katika siku za mwisho watakuwa wanazishika amri za Yahweh (Ufunuo 12:17 na 14:12). Kutokana na Maandiko haya, tulikuwa na hakika kabisa kwamba

***Si kukariri sikuzote ambako hufanya tofauti katika kukumbuka Maandiko. Badala yake, kukumbuka pia inamaanisha, kufikiria kuhusu mambo ambayo umesoma hivi punde na kuyapitia kwa bidii, ili yabaki safi kila wakati akilini mwako.***



wale wasiozishika amri za Yahweh hawataingia Yerusalemu mpya, au kupewa haki ya kula kutoka kwa mti wa uzima (Ufunuo 22:14). Lakini, cha ajabu, tunaposoma kutoka kwa maandishi ya Agano Jipya ya Paulo, mashaka ya zamani, ya zamani juu ya kushika sheria za Yahweh mara kwa mara yalijitokeza katika akili zetu. Je, tuliondoaje mashaka haya.

Kwanza, tuliamua kusoma sheria ya Yahweh yenyewe na kuona uadilifu ulio ndani yake. Baada ya kuzama katika kujifunza kwa sheria za Yahweh kwa miezi kadhaa, tuligundua kwamba lazima kuwe na majibu ya kimantiki kwa mapingamizi yanayoonekana ya Paulo kwa kushika sheria. Hatua yetu iliyofuata ilikuwa kuchunguza maandishi ya Kiyahudi ya kisasa ili kugundua kile kingehusiana na kile ambacho Paulo (Mbenyamini, Myahudi, Mfarisayo) alisema. Kwa kushangaza, wakati maandishi ya Paulo yalipolinganishwa kwa ukaribu na mandishi ya talmudi, majibu yakawa mara moja. Kisha utakaso wetu wa kiakili kutoka kwa mafundisho ya uwongo yenye kusumbua ukawa rahisi.

Hatua ya tatu njiani ya kupata utafiti wa Biblia wenye faida ni kuchagua toleo nzuri la funzo la Biblia. Karibu mwanzoni mwa kujifunza kwetu kwa Biblia kwa bidii, nilipata **Companion Bible**. Biblia hii ni nakala ya **King James** yenye maelezo mengi na marejeleo mbalimbali yanayoruhusu ufikiaji tayari wa maneno ya Kiebrania na Kigiriki ambayo huathiri maana ya tafsiri. Mengi ya maneno hayo yalitafsiria kwa makosa, na tafsiri sahihi itachangia sana kupatanisha Biblia.

Hata hivyo, mtu hapaswi kusimamia hapa. Anapaswa kupata tafsiri kadhaa za Biblia bora zaidi, za kisasa ambazo zimethibitishwa kuwa sahihi kuliko **King James version**. Mojawapo ya hizo ni **American Standard version 1901.** Toleo hili, hadi leo linashikilia nafasi ya kipekee katika miduara ya kitheolojia ya kihafidhina. Pengine ni tafsiri bora zaidi, halisi ya Biblia kuwahi kutolewa. **The Bible**, **American Translation**, kawaida ikijulikana kama **Smith-Goodspeed**, ni kazi nyingine bora iliyofanywa na kikundi cha wahariri. The **New English Bible** ina sifa ya usahihi wa kipekee katika sehemu ya Agano Jipya. Msaada wa thamani sana kwa masomo ya Agano Jipya ni **Benjamin Wilson Emphatic Diaglott**.

Mtu lazima asipuuze kupata konkordansi nzuri. Imesemwa kwamba **Cruden's Concordance** ni ya waumini wa kawaida, **Young's Concordance** kwa waumini wachanga, na **Strong's Concordance** kwa waumini wenye nguvu. Kila mojawapo ya visaidizi hivi vya utafiti vilivyobainishwa ina sifa zake binafsi. Inaweza kusemwa kwamba **Strong's Concordance** ndiyo iliyo rahisi zaidi kutumia, na ndiyo bora zaidi kwa utafiti wa Biblia.

Konkodansi kamilifu zitamsaidia mtafutaji wa Ukweli katika masomo ya maneno. Inapendeza, inaelimisha, na inatia nuru kuona jinsi maneno yametafsiriwa kwa njia tofauti katika vifungu mbalimbali vya Biblia. Hata hivyo, tunapaswa kuwa waangalifu kuruhusu uwezekano wa homonimu kati ya maneno ya Maandishi ya awali, huku tukizingatia maana ya maneno yanayofanana (*parallismus membrorum*). Ni lazima pia tuwe waangalifu kukubali tofauti ndogo za kileksia katika minyambuliko ya maneno, kwa kuwa kila mtu hawezi kufanya kazi kama mamlaka kuu juu ya lugha ambayo hajajifunza kuzungumza.

Kadri mhariri anavyozidi kujifunza Neno la Yahweh kwa kina, ndivyo anavyokuwa mwenye heshima na tahadhari zaidi anapokaribia maandiko ya Biblia. Neno hili la tahadhari lazima lipitishwe kwa wasomaji wa **The Sacred Name Broadcaster**. Juhudi za kutafsiri za karne nyingi, na fafanuzi za mambo ya kale haziwezi kuachwa kirahisi, kwa sababu nyingi ya tafsiri hizi zilifanywa chini ya mamlaka ya wale walioishi wakati wa Yahshua Messiah.

Usomaji wa kudumu wa Maandiko ni hatua inayofuata katika njia ya kujifunza Biblia vizuri. Kila mtu anapaswa kujaribu kusoma Biblia mara kwa mara- ikiwa ataweza kusoma kitabu hicho ndani ya muda ufaao. Kumbuka KUSOMA Biblia na sio maoni tu kuhusu Biblia.

Mapema katika huduma hii, mtu mmoja (kwa uharaka fulani) alilalamika kwamba tulikuwa tukichapisha nakala zisizotosha ili kumfanya yeye aendelee katika nyenzo za kusoma. Jibu langu lilikuwa, “Soma Biblia.” Chanzo ambacho maelezo yote ya Maandiko hatimaye yametolewa ni maandishi yaliyovuviwa. Tunapaswa pia kuwa waangalifu kupunguza mambo tunayosoma nje na kukazia fikira nakala zinazofundisha mafundisho yenye uzima, au Biblia yenyewe. Vinginevyo, msomaji atachanganyikiwa. Kushikamana na chanzo (source) hakuwezi kuwa na madhara, lakini kutakuwa na athari ya kuleta utulivu kwa mwanafunzi.

Hatua inayofuata ni kutafakari ulichosoma. Ili kukumbuka mambo unayosoma, itahitaji kufikiri na kutafakari juu ya yale unayojifunza, kwa kugawanya akilini mwako kwa uaminifu ukweli ambayo unajifunza. Mara nyingi sana, mtu hakazii fikira vya kutosha juu ya kile anachosoma, na kwa hiyo, ndani ya saa 24 anasahau zaidi ya asilimia 90


ya nyenzo. Vitu vingine vingi vinashindana kwa umakini wetu wa kiakili. Zingatia kitabu maalum unachosoma na ukazie fikira habari inayozungumziwa katika kitabu hicho.


Si kukariri sikuzote ambako hufanya tofauti katika kukumbuka maandiko. Badala yake, kukumbuka pia inamaanisha, kufikiria kuhusu mambo ambayo umesoma hivi punde na kuyapitia kwa bidii, ili yabaki safi kila wakati akilini mwako.


Ili kufaidika zaidi na kujifunza Biblia, ni lazima uzae matunda kwa kutumia mafundisho ya neno katika maisha yako ya kila siku. Utii ni tunda la kusoma. Mwenyenguvu Yahweh ametujulisha kwamba atawapa Roho Mtakatifu wale wanaomtii. ***"Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu ambaye Yahweh amewapa wote wamtiio."*** (Matendo 5:32). Kwa kuweka katika vitendo mambo unayojifunza, utapokea zaidi Roho mtakatifu wa Yahweh na, hivyo, kukua katika neema na maarifa.


Wasomaji wengi wa jarida hili wameuliza swali, "Ulijifunzaje mambo yote mazito unayotangaza?" Jibu rahisi ni kwamba mambo haya yalifunuliwa kwetu na Baba wa Mbinguni kupitia Roho Wake Mtakatifu. Katika siku hizi za mwisho, Mwenye-nguvu Yahweh ametupa baraka hii kuu ya ufahamu uliopanulia ili kuweza kuwa wa huduma bora kwake. Yahweh anatamani wote waelewe Biblia katika siku hizi za mwisho kama shahidi wa ukuu Wake. Nabii Danieli ametuambia kwamba waaminifu watafanya mambo makuu. Imani yetu inapofungwa kwa usalama kwenye mwamba wa kweli hakuna shambulio la kishetani litakaloiharibu.


Ikiwa ungependa kupata ufahamu wa Biblia, wazee wa Assemblies of Yahweh wanatamani kukutumikia. Je, tunaweza kusikia kutoka kwako hivi karibuni? Kadri unavyochukua hatua haraka, ndivyo upesi utakavyopokea baraka za Yahweh na uhusiano wa karibu wa kibinafsi unaoweza kusitawisha Naye. SNB




Kwa maelezo ya bei andika kwa:
***Assemblies of Yahweh***
***PO Box C***
***Bethel, PA 19507***
***(717) 933-4518***
***www.assembliesofyahweh.com***



# Zawadi yetu kwa Ulimwengu

# Maarifa ya Neno la Uzima

Mara kwa mara, katika jarida la **The Sacred Name Broadcaster**, tuliuliza ikiwa wasomaji wanathamini maarifa wanayopokea kupitia uchapishaji huu. Tunaweza kwa furaha kuripoti kwamba mamia ya barua zimepokewa hapa Bethel kutoka kwa wasomaji ambao walitoa shukrani za dhati kwa juhudi zetu katika kuchapisha jarida **la The Sacred Name Broadcaster**.

**na Mzee Jacob O. Meyer**

Kwa mtazamo wetu, ni wazi tuko kwenye kilele cha ***mdororo mkali wa uchumi***. Sio tu mfumuko wa bei unaotokea katika Marekani, lakini mataifa mengi ya kigeni yameathiriwa sana na hali duni ya kiuchumi na mfumuko wa bei unaoongezeka.

Hili linamaanisha kwamba huku watu wengi wakipoteza ajira zao, au wanapunguziwa saa zao za kazi, zaka na matoleo yanayotumwa Bethel kuunga mkono huduma hii yamepunguzwa. Kwani hiyo zaka inategemea juu ya mapato au ongezeko ya kila mmoja wa watu wa Yahweh (tazama Walawi 27:30-33), wakati mapato ya mtu binafsi yanaenda chini, zaka na matoloe yanayopokewa kwa huduma ya Yahweh pia hupunguzwa baadaye.

Tumekuwa tukiwaelezea ndugu katika mahubiri yetu ya Sabato, pamoja na sehemu ya kipengele cha “Mwelekeo wa Kinabii” katika jarida la **The Sacred Name Broadcaster**, kwamba AJALI MBAYA YA KIUCHUMI DUNIA LAZIMA itokee ili kwamba mfumo wa Mnyama wa Ufunuo 13 unaweza kuzinduliwa. Serikali hii ya Mnyama itakuwa chini ya utawala wa mtu ambaye atadai kuwa na majibu yote kwa matatizo na kutafuta kurejesha nyakati nzuri kwa ulimwengu. Dini za kidunia







kwa haraka zitaunga mkono mtu huyu, kama zitakavyofanya taasisi zingine za kidunia. Hata hivyo, atapendekeza tu mfumo wa uchumi wa pamoja, ambao hautategemea juu ya utendakazi na ufanisi wa hali ya juu wa mfumo wa uchumi wa Mwenye-nguvu Yahweh. Kwa hiyo, mfumo wa mnyama utaanguka hivi karibuni, na ulimwengu utakuwa katika hali mbaya zaidi kuliko hapo awali, na hivyo kulazimisha Ujio wa Pili wa Yahshua aliye Messiah.

Mfumo wa Mnyama wa Ufunuo mlango wa 13 ni dhahiri utajengwa juu ya kukataa kwa njia ya maisha ya Mwenye-nguvu Yahweh, kama ilivyofunzwa katika Torati (Sheria) Yake. Mfumo huu wa Mnyama UTAZIKANA AMRI za Yahweh katika kupendelea za serikali moja ya umoja ya dunia. Wanasiasa wametumia neno *utaratibu mpya wa dunia* (New world Order)katika matukio mengi, na bado wameshindwa kufafanua maadili yake. Mnyama atakuja eneo la tukio akiwa na mpango, lakini atasisitiza juu ya kutengwa kwa Neno la Mwenye-nguvu Yahweh, Torati (sheria) Yake, na amri. Kukataliwa vile kwa moja kwa moja kwa Sheria ya Yahweh kutalazimisha alama ya Mnyama.

Assemblies of Yahweh imeteuliwa na Mwenye-nguvu Yahweh kuchukua ujumbe huu wa onyo kwa ulimwengu. Katika Malaki 4:4-6, tunaarifiwa kuhusiana na ujumbe ambao utahubiriwa kwa miisho ya dunia kabla tu ya Messiah kurudi. Ujumbe unawahimiza watu wote ambao wana hamu ya Ukweli kukumbuka Sheria ya Musa, ambayo Yahweh alimwamuru katika Horebu. Hili linamaanishaTorati, Maandiko Matakatifu yaliyoandikwa na Musa, ambayo yako na amri za Yahweh. Kumbuka, Mwenye-nguvu anaweka alama juu ya wale ambao wanamtii Yeye (Ezekieli 9). Leo, amri za Yahweh zimekataliwa. Watu hawana aibu! Wanamkaidi Mwenye-nguvu Yahweh kwa kukiuka Sheria Zake bila kuadhibiwa. Inaonekana kana kwamba watu wa ulimwengu kwa kweli wanatamani kuwa waovu, badala ya kutafuta Sheria za Yahweh, na hivyo kuishi.

Kipengele cha pili cha ujumbe huu wa onyo wa wakati wa mwisho unaoenda hadi miisho ya dunia ni kuelezea kwamba kutakuwa na Mwenye-nguvu MMOJA wa Kweli Aliye Hai na kwamba Jina Lake ni Yahweh. Nabii EliYah atatangaza ujumbe huu katika siku za mwisho, akija kwa nguvu na roho wa nabii ambaye maisha yake tunapata yamerekodiwa katika 1 Wafalme sura ya 17 hadi 2 Wafalme sura ya 2. Jina lake EliYah linamaanisha- **Mwenye-nguvu Wangu ni Yahweh**. Ujumbe huu wa Jina Takatifu utaenda nje kwa miisho ya dunia. Ujumbe sambamba wa Maandiko ambao unaelezea hili kabisa unaweza kupatikana katika Ufunuo sura ya 14. (Umesoma maandishi yaliyochapishwa na Assemblies of Yahweh juu ya mada ya fundisho la Jina Takatifu? Kama sivyo, andika mara moja kwa nakala. Ni bure kwa wanaouliza. Andika kwa Assemblies of Yahweh, PO Box C, PA 19507.)

Huduma ya Assemblies of Yahweh ilianza kama punje ndogo ya haradali katika 1966. Ujumbe kwanza ulienda nje kupitia kituo kimoja cha matangazo, na kisha ukaendelea kukua hadi Ukweli wa Yahweh umeweza kutumwa kwa miisho ya dunia kupitia robo karne iliyopita.

Katika mapema 1980, tulianza ujenzi wa kituo cha redio cha mawimbi mafupi hapa Betheli. Ujenzi huo ulikamilishwa katika 1984. Sikiliza kwa www.wmlk.net kwa sehemu yako ya kila siku ya mafundisho ya Biblia.

Ingawa mawimbi ya kituo cha redio cha WMLK yana lengo la eneo la Ulaya na Mashariki ya Kati, mawimbi yatasikika kwa wazi katika maeneo mengine mengi ya ulimwengu. Kwani tunatangaza kutoka Marekani, inasikika hapa katika Marekani. Wasikilizaji katika maeneo mengi ya Marekani wameweza kuchukua mawimbi yetu ya mara kwa mara. Maeneo mengi ya Kanada yameweza kusikia matangazo vizuri sana. Kwani mawimbi husafiri njia ya




***Huduma ya Assemblies of Yahweh kwa hakika ni kazi ya dhabihu na upendo kwa watu ambao hawajapata fursa ya kujifunza maarifa ambayo yatawaletea wokovu.***

duara ya kimataifa, majimbo ya baharini ya Kanada yameweza kupokea mawimbi ya WMLK vizuri sana. Pia tumegundua kuwa antenna ya kituo ina sehemu za nyuma na kando zinazovuka kaskazini magharibi mwa Kanada, Karibiani, na kusafiri katika eneo la kusini magharibi mwa Marekani.

Mbali na kituo cha Redio cha WMLK, tunatangaza kwenye mtandao wa vituo vya redio vya kibiashara. Baadhi ya vituo vya redio vyenye nguvu katika Marekani na nchi za kigeni vinabeba **Matangazo ya Jina Takatifu**, na tunaamini kwamba utasoma logi ya redio katika **The Sacred Name Broadcaster** ili kubaini ikiwa unaweza kusikiliza kwa **Matangazo ya Jina Takatifu** katika mtandao wetu wa vituo vya kibiashara.

Moja ya milango mikubwa iliyo wazi kwa ufikiaji na Assemblies of Yahweh ni machapisho ya Assemblies of Yahweh. Tunachapisha jarida la **The Sacred Name Broadcaster**. Tunatuma kwa njia ya barua maelfu ya bidhaa za maandishi kila mwezi.


Mtandao, www.assembliesofyahweh, ni chombo muhimu na chenye ufanisi. Watu wanaovutiwa wanaweza kutazama machapisho ya Assemblies of Yahweh na, pia kusikiliza kwa mtiririko wa moja kwa moja.

Mwaka huu tulizindua programu isiyolipishwa ambayo inapatikana kwa kupakuliwa kutoka Apple Store au Google Play Store. Habari na maagizo ziko kwenye ukurasa wa 19 wa toleo hili la **The Sacred Name Broadcaster**.


Uharaka wa wakati huu, kama tunavyouona, ni kufanya Ukweli huu wa kupatikana kwa watu wengi zaidi kote duniani kabla ya matukio ya janga la mwisho wa enzi kutufikia. Marafiki, tungependa kupanua ufikiaji wetu! Assemblies of Yahweh, katika hatua hii ya historia ina shirika kubwa sana mahali pake. Ni maombi yetu kwamba Mwenyenguvu Yahweh atatuongoze mbele kwa njia za miujiza ili Ukweli wake uweze kuwasilishwa kwa watu wengi zaidi ulimwenguni kote kabla hajakusudia kuhukumu mfumo huu wa kilimwengu wa Babeli tunamoishi.

Hatujawahi kuomba michango tangu Assemblies of Yahweh ilipoanza. Limekuwa zoea letu kunapokuwa na uhitaji, kuweka uhitaji huo mbele ya akina ndugu waliobatizwa wa Assemblies of Yahweh na wale wafanyakazi wenzetu waaminifu wanaotegemeza huduma hii mara kwa mara. Katika toleo hili la **The Sacred name Broadcaster**, kwa hivyo tunataja kwamba mahitaji yapo wakati huu kwa Assemblies of Yahweh. Moyo wako ukiguswa, tunakualika utusaidie kupeleka Ukweli huu kwa wengine.


Kwanza kabisa, tunatumai kuendelea kutangaza ujumbe wa wokovu kwa njia ya televisheni. Tulianza utangazaji wa televisheni mwaka wa 1974, ambapo ilienda katika hali ya kusimamishwa kwa muda mwaka wa 1981. Tumenunua vifaa bora zaidi vya kutangaza **The Sacred Name Telecast**, na tunanuia kuendelea kufanya matangazo. Hata hivyo, ununuzi wa muda wa hewani uta-




Swahili




French




Spanish

The Sacred Name Broadcaster inapatikana pia katika miundo ya lugha nyingi

hitaji dhabihu kubwa kwa huduma hii. Kwa hivyo, tunaweka hitaji hili mbele ya familia ya wasomaji wa **The Sacred name Broadcaster**.

Tena, kusisitiza, hatuombi pesa, lakini badala yake, mahitaji haya yanawekwa mbele ya wasomaji wa jarida la **The Sacred Name Broadcaster**. Ikiwa Mwenye-nguvu Yahweh ataweka juu ya moyo wako kuchangia, tunajua kwamba Yeye atawabariki wale wanaofanya. Sisi si kama huduma zingine- tunapofikisha hitaji kwa akina ndugu, hitaji hilo ni la kweli, lakini tutaendelea kufanya Ukweli huu upatikane bila malipo kwa wote watakaoupokea.

Huduma ya Assemblies of Yahweh kwa hakika ni kazi ya dhabihu na upendo kwa watu ambao hawajapata fursa ya kujifunza maarifa ambayo yatawaletea wokovu. Nabii Hosea anaomboleza kwa sauti ya Mwenye-nguvu Yahweh ***"Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa: kwa kuwa wewe umeyakataa marifa, mimi nami nitakukataa wewe, usiwe kuhani kwangu mimi: kwa kuwa umeisahau sheria ya Elohim wako, mimi nami nitawasahau watoto wako. Kadri walivyozidishwa, kwa kadiri iyo hiyo walinitenda dhambi: nami nitageuza utukufu wao kuwa aibu."***(Hosea 4:6-7).

Kwa hiyo, nyakati ambazo tunaishi sasa zinatupa sababu ya kuhangaikia wale ambao hawaijui Kweli ya Yahweh. Tunajitahidi kupeleka Ukweli huu hadi misho ya dunia tukitumai kwamba watu watasikia na kukumbatia mafundisho ya uzima ya Neno la Yahweh na kujitayarisha wenyewe kumlaki Yahshua Messiah hewani, atakaporudi. Kuongezea, katika nyakati hizi zenye misukosuko ya kiuchumi, watu watakuwa na fursa kujifunza ukweli wa Neno kabla ya mashambulizi ya mfumo wa Mnyama, ili waweze kujenga Sabina yao ya kiroho ya usalama.

Leo ujumbe wa Assemblies of Yahweh unaenea ulimwenguni kote kwa sauti inayoongezeka. Kama unavyojua, kila kitu ambacho lazima tununue leo kinagharimu pesa nyingi. Hakuna kitu cha bure! Hakuna chakula cha mchana cha bure; mtu hulipia chakula hicho cha "bure" cha mchana- ingawa kinatolewa bila malipo.

Ndivyo ilivyo pia kwa huduma ya Assemblies of Yahweh. Ingawa tunatoa uandikishaji wa mwaka mmoja wa jarida hili bila malipo kwa yeyote anayeandika na kuiomba, mtu fulani anapaswa kulipia gharamu za uchapishaji. Mtu hulipa gharama za kuchapisha upya makala na vitabu, na **The Sacred Scriptures**, *Bethel Edition Bible*. Yahshua Messiah ametuambia, "mmepokea bure, toeni bure." Wale wanaolipa gharama za uchapishaji wa machapisho ya ufikiaji ya Assemblies of Yahweh ni washiriki na watenda kazi wenzi wanaotoa zaka matoleo yao kwa hiari ili huduma itolewe kwa mahitaji yake.

Ni furaha yetu kukuhudumia na kukutumia maandishi yanayochapishwa na Assemblies of Yahweh. Maandishi tunayotoa hutumwa bila malipo, na tuna-

*Continued on page 19.*

## Sehemu 1




# Alama ya Yahweh Dhid

**na Mzee Jacob O. Meyer**

Nimesema kwa muda mrefu sana kwamba kuanguka kwa uchumi kunakuja kwa ulimwengu wa Magharibi. Marekani na Ulimwengu wa Magharibi, kwa jambo hilo, zimechukuliwa na utumaji wa pesa wa kielektroniki. Mingi ya shughuli zetu za kifedha zinafanywa kijiditali. Fedha, inaonekana hutumiwa mara chache, kwa sababu kuteleza kidole, kugonga, kwa kadi ni rahisi zaidi. Sarafu, kama unavyoijua itaweza kubadilishwa na Fedha za Kidijitali za Benki Kuu- CBDC. Serikali ijayo ya Mnyama, ambayo itachukua nguvu, itahakikisha hili. Kama tunavyoona katika Ufunuo mlango wa 13, serikali ya Mnyama itakuwa katika udhibiti kamili wa mfumo wa fedha, kukubali au kukataa kila muamala, pamoja na ukusanyaji wa kodi yoyote katika mahali pa mauzo.

Katika Ufunuo 13:16, ***"Naye awafanya WOTE, WADOGO kwa WAKUBWA, MATAJIRI kwa MASKINI, na WALIO HURU kwa WATUMWA, WATIWE CHAPA katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba awaye yote ASIWEZE KUNUNUA WALA KUUZA, isipokuwa ana CHAPA ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake. Hapa ndipo penye hekima, Yeye aliye na akili, na aihesabu hesabu ya mnyama huyo; maana ni hesabu ya binadamu. Na hesabu yake ni mia sita, sitini, na sita."*** Alama ya Mnyama ni nini hata hivyo? Kuna maswali mengi na maoni yasiyo na idadi yanayotolewa kuhusu Alama ya Mnyama. Baadhi ya watu wanafikiria itakuwa alama halisi juu ya watu wa ulimwengu huu- uandishi wa aina fulani- au pengine nambari iliyochorwa kwa wino usioonekana ambayo itahitaji *laser* kuisoma. Baadhi wanafikiria itakuwa nambari ya aina fulani ambayo tutapokea, au *chip* ya kompyuta, au mfumo wa hifadhi ya jamii, pamoja na nambari yake inayohusika. Wengi wanafikiria kwamba alama ya Mnyama ni kompyuta.

Ninakumbuka nilipopokea nambari yangu ya siri PIN (Nambari ya Kitambulisho cha Ki-



# li ya Alama ya Mnyama

binafsi) kwa kadi yetu ya kwanza ya plastiki ya benki, mimi na bibi yangu tulipewa wote barua yenye maelezo ya PIN. Nilipompa barua, tuligundua kwamba alikuwa na nambari tofauti na mimi, hata ingawa tulikuwa na akaunti ya benki ya pamoja. Hivyo,sisi kila mmoja wetu alikuwa na nambari yetu ya kitambulisho ya kibinafsi ya kufikia akaunti yetu ya pamoja. Niliiona ni ya kuvutia kwamba kila mmoja wetu alikuwa na kitambulisho cha kipekee kufikia akaunti sawa. Ingeonekana isiyowezekana miaka iliyopita, wakati zama za kompyuta zilianza, kwamba kila binadamu juu ya uso wa dunia angezuiliwa kutoka kwa shughuli ya kifedha kwa amri ya serikali ya Mnyama. Teknolojia ya kompyuta kutimiza unabii huu iko hapa.

Kama tutaangalia kwa neno *alam*a katika Ufunuo 13:16, tunapata katika Kigiriki kwamba neno ni *charagma*. Linamaanisha *mkwaruzo, au mchongo, muhuri au beji ya utumwa*, katika **Strong's Concordance**. Neno *charagma* ni tofauti kwa kitabu cha Ufunuo, likipatikana hapo mara saba. **Arndt and Gingrich Greek Lexicon**, inaonyesha kwamba inapaswa kutafsiriwa kama *chapa* au *muhuri*. Wanaionyesha kutoka kwa hati zingine kadhaa za kale za Kigiriki kama chapa, kama vile juu ya farasi. *Charagma* linatumika kwa chapa juu ya farasi, kama muhuri kwenye hati, na maonyesho kwenye sarafu. PIA INAIFAFANUA KAMA PICHA. Kwa hiyo, Mnyama pia ana alama YAKE- mchongo wake au beji yake ya utumwa. Kama chapa ambayo itawekwa juu ya watu, hii itakuwa **alama ya kitambulisho cha kibinafsi** ambayo Mnyama atatia chapa kwenye AKILI ya watu.

Yahweh pia anayo alama Yake ya utambulisho anayoiweka juu ya watu Wake. Maandiko ya Agano la Kale kwa mfano, yanatuambia alama ya Yahweh itakuwa nini. ***"MTIE ALAMA MTU MKAMILIFU, umtazame mtu mnyofu, maana kuna mwisho wa furaha kwa mtu huyo wa amani. WAKOSAJI WATAANGAMIZWA pamoja: Wasio haki mwisho wao WATAHARIBIWA."*** (Zaburi 37:37-38). Ni wazi kuna alama kwa WATU WA YAHWEH. Hata hivyo, kinyume kwa alama ya Yahweh, kutakuwa na alama ya

**Yahweh ni Elohim wetu, na yeye ndiye Mwenye nguvu wetu. Yahweh ndiye aliye na nguvu ya kutosha kutenda kwa niaba yetu.**

kipekee ya Mnyama. Hizi ni alama mbili ambazo zinatajwa katika Maandiko. Alama ya Yahweh ni alama ya UTII, wakati alama nyingine ni alama ya UVUNJAJI SHERIA- alama ya **UOVU**. Neno kwa *alama* katika Zaburi 37:37 ni #8104 katika **Strong's Exhaustive Concordance** na ni kitenzi cha Kiebrania *shamar*. Linamaanisha *kuzunguka, kulinda au kulinda, au kuhudumia*.

***"Na WOKOVU wa wenye haki una Yahweh: yeye ni NGOME yao wakati wa TAABU."*** (Zaburi 37:39). Yahweh ni nguvu yetu katika wakati wa shida. Hili linatuelekeza kuelekea kwa DHIKI ya wakati wa mwisho. Neno la taabu, katika mstari huu, ni *tsarah* ambalo ni neno la ***dhiki*** katika Agano la Kale. Neno la mzizi kwa *tsarah* ni *tsar*, ambalo linamaanisha *mahali pembamba au mahali pa kubanwa*, kwa njia ya mfano *shida*. Linatafsiriwa kama *adui, dhiki, uchungu, dhiki, na shida*. Katika Kigiriki, neno kwa *dhiki* ni *thlipsis* ambalo linamaanisha *shinikizo, uchungu, mateso, dhiki na shida*.

***"Naye Yahweh huwasaidia na kuwaopoa: huwaopoa na wasio haki na kuwaokoa kwa kuwa wamemkimbilia yeye."*** (Zaburi 37:40). Natamani tungeweka kifungu hiki katika akili na mioyo yetu. Kifungu hiki tofauti kinaonyesha **utengano** kati ya watu **waadilifu** na watu **waovu** duniani. **Wenye haki** watawekwa alama ya Yahweh.**Waovu** pia watawekwa alama vilevile. Katika Mathayo 25, Yahshua anaelezea kwamba kutakuwa na **utengano** kati ya kondoo na mbuzi, ambao utafanyika katika kurudi kwake, atakapousimamisha Ufalme wa Yahweh.

**Alama ya Mikate Isiyotiwa Chachu**

Katika Kutoka 13, tunapata muunganisho kati ya alama ya Yahweh na alama ya Mikate isiyotiwa Chachu. Kifungu hiki ni Maandiko ya msingi kwa somo hili, kufafanua alama ya Mnyama. ***"Musa akawaambia hao watu, kumbukeni siku hii, mliyotoka nchi ya Misri, kutoka nyumba ya utumwa; kwa kuwa Yahweh aliwatoa mahali hapa kwa nguvu za mkono wake: na usiliwe mkate uliochachwa."*** (Kutoka 13:3). Tumeagizwa kukumbuka siku ambayo Yahweh alitutoa kutoka Misri yetu ya dhambi, kwa sababu, kwa nguvu ya mkono, Yahweh alisonga na kutenda KWA NIABA YETU KAMA WAISRAELI. Ni lazima tukumbuke kwamba kuna uhusiano tofauti kati ya neno *Elohim* na neno *nguvu* ambalo linatumika hapa. Yahweh ni Elohim wetu, na yeye ndiye Mwenye nguvu wetu. Yahweh ndiye aliye na **nguvu ya kutosha** kutenda kwa niaba yetu. Baadaye, maneno *Elohim* na *nguvu* yanahusiana waziwazi, kama Yahweh ni mwenye nguvu wetu, Mwenye nguvu.

***"Mtakula mikate isiyochachwa muda wa siku saba, nayo siku ya saba itakuwa ni sikukuu ya Yahweh. Mikate isiyochachwa italiwa katika hizo siku saba, mkate uliotiwa chachu usionekane kwako, wala chachu isionekane kwako, ndani ya mipaka yako yote. Nawe utamwambia mwanao siku hiyo, ukisema, ni kwa sababu ya hayo Yahweh aliyonifanyia hapo nilipotoka Misri. Nayo itakuwa ISHARA kwako katika mkono wako, na kwa UKUMBUSHO kati ya macho yako, ili kwamba SHERIA YA YAHWEH ipate kuwa KINYWANI mwako: kwani Yahweh alikutoa utoke Misri kwa mkono wenye uwezo. Kwa hiyo utaitunza amri hii kwa wakati wake mwaka baada ya mwaka."*** (Kutoka 13:6-10). Elohim, Aliye na nguvu, anaweka alama (ishara) juu ya mkono wetu wa kulia, na ukumbusho (ukumbusho) kati ya macho yetu, katika vipaji vya nyuso zetu. Kama vile Mnyama anavyoweka alama juu ya watu wake, Yahweh pia anaweka alama, anapomweka alama mtu mkamilifu ambaye anashika Sheria Yake- ambaye ni mtiifu kwake- ambaye ana kiwango cha haki na kuishi nacho.

Sasa mbele kidogo katika mstari wa 16, neno ishara ni *'owth* kumaanisha *alama, muujiza, ishara na bendera*. ***"Jambo hilo litakuwa ni ishara mkononi mwako, na utepe katikati ya macho yako; kwa kuwa Yahweh alitutoa Misri kwa uwezo***






***wa mkono wake.”*** (Kutoka 13:16). Kwa kushika siku za Mikate Isiyotiwa chachu, tunafanya msimamo. Tunasema kwamba tunashika siku takatifu za YAHWEH kinyume na kuweka SIKU TAKATIFU ZA DUNIA.

Katika Assemblies of Yahweh, hatuna uwakilishi wowote wa Yahweh katika kumbi za mikutano, au maeneo ya ibada, isipokuwa kwa Tetragrammatoni. Herufi nne (ambazo ni vokali, kulingana na Josephus) ambazo hujumuisha Tetragrammatoni ndiyo uwakilishi wa pekee tulio nao kwa Yahweh. Tunamwabudu Yahweh- Elohim pekee wa Kweli aliye Hai- Mwenye-nguvu asiyeonekana. Hatuna sanamu ya kutisha inayosimama mbele ya chumba, ikiamuru umakini wetu, ikidai kwamba tutumikie sanamu ya kuchonga. Hata hivyo, TULICHONACHO NI NENO LAKE, na Neno Lake limeweka hofu na heshima kwake katika mioyo yetu. Hatupaswi kuwa na sababu nyingine kwa nini tuko hapa isipokuwa kwamba tuwe na upendo kwa Neno Lake.

Katika Assemblies of Yahweh, hatuna uwakilishi wowote wa Yahweh katika kumbi za mikutano, au maeneo ya ibada, isipokuwa kwa Tetragrammatoni. Herufi nne (ambazo ni vokali, kulingana na Josephus) ambazo hujumuisha Tetragrammatoni ndiyo uwakilishi wa pekee tulio nao kwa Yahweh. Tunamwabudu Yahweh- Elohim pekee wa Kweli aliye Hai- Mwenye-nguvu asiyeonekana.


Wazo hili linaendelezwa katika Kumbukumbu la Torati 6, ambacho ni kifungu kinachopendwa kwa kila mmoja wetu. ***“Na hii ndiyo sheria, na amri, na hukumu, alizoziamuru Yahweh, Elohim wenu, mfundishwe, mpate kuzitenda katika nchi ile mnayoivuka kuimiliki; upate kumcha Yahweh, Elohim wako, KUSHIKA AMRI zake zote, na SHERIA zake, ninazokuamuru, wewe na mwanao, na mwana wa mwanao, siku zote za maisha yako, tena siku zako ziongezwe. Sikiza basi, Ee Israeli, ukaangalie kuzitenda upate kufanikiwa, mpate kuongezeka sana, kama Yahweh, Elohim wa baba zako alivyokuahidi, katika nchi ijaayo maziwa na asali.***

***“Sikiza, Ee Israeli: Yahweh ni Elohim wetu, Yahweh ni mmoja: Nawe MPENDE Yahweh Elohim wako kwa moyo wako wote, na kwa nafsi yako yote, na kwa nguvu zako zote. Na MANENO HAYA, ninayokuamuru leo yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako. Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako.”*** (Kumbukumbu la Torati 6:1-9).

Mstari wa 3 unatuelekeza kwamba kama **tutasikia na kuangalia**- kumtii Yahweh- ameahidi kwamba tutaongezeka. Kwa hiyo, lazima tushike Sheria ya Yahweh. Ikiwa hatutatii, tutapungua na kulaaniwa. Ni kwa nini kwamba tunatii amri za Yahweh? SIO kwa sababu tuna sanamu ya kuchonga, ambayo inatia hofu mioyoni mwetu, kutulazimisha kuanguka chini mbele yake na kuabudu. Hapana! Ni kwa sababu TUNAMPENDA Yahweh na tunampenda KWA MOYO WOTE- **kwa moyo wetu wote**, **nafsi, na nguvu**. Yahweh ametuamuru kwamba **Neno** lake litakuwa juu ya MIOYO YETU.

Katika Kutoka 13, tumejifunza kwamba sheria ya Yahweh iko

midomoni mwetu tunapotunza Mikate Isiyotiwa Chachu. Hilo ndilo Mikate Isiyotiwa Chachu inasimamia- mafundisho safi- utunzaji wa amri za Yahweh na sheria. Sheria hizi hazipaswi kuwa tu za nje, hiyo ni, kuandikwa juu ya meza za mawe, lakini ni za **kuandikwa juu ya mioyo yetu**. Kuna mwanamume Myahudi ambaye aliniuliza kama ninavalia filakteria. Nilimjibu kwa kumuuliza, "*Ni wapi unasoma katika Biblia kwamba lazima uvalie filakteria*?" Kisha alijibu, "*Katika Kumbukumbu la Torati 6, shema inatuambia tufanye hilo*." Nilimwambia (na tabasamu usoni mwangu), "*Mnakosea kwa kutojua Maandiko.Haujasoma katika Kumbukumbu la Torati 6:6*, ***"Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako."*** Haituambii kwamba lazima tuvalie **filakteria za kimwili**, lakini ina maana ya KINA zaidi kuliko hili. Ina maana ya KIROHO kwa kila mmoja wetu. Ikiwa neno la Yahweh liko mioyoni mwetu, TUTALIPENDA Neno, KULISHIKA Neno, na KULITII Neno. Ikiwa Neno la Yahweh liko MOYONI mwetu, basi neno la Yahweh litaelekeza mikono yetu na kuweka mikono yetu kutokana na mabaya. Sheria ya Yahweh kama **utepe katikati ya macho yetu**, linamaanisha kwamba njia yetu ya kufikiria na michakato yetu ya mawazo itakuwa inayodhibitiwa kulingana na amri za Yahweh. Kuyaandika **juu ya miimo ya nyumba** yako inamaanisha kwamba milango ya nyumba yetu ya kiroho, ambayo ni macho, masikio, mdomo, na mapua. Kwa mfano, yale tunayoona na tunayosikia yanaingia kwenye akili zetu.



***Chochote tunaruhusu katika akili zetu hatimaye kitatoka katika matendo yetu. Yahshua Messiah alifundisha yale yaliyo akilini mwetu na katika mioyo yetu hatimaye yatafichuliwa katika matendo yetu.***

Katika zama hizi za kompyuta, kuna msemo: "*Takataka kuingia ndani, takataka kutoka nje*." Chochote kilichopangwa ndani ya kompyuta ndicho kitatoka; hivyo, ukweli mzuri ulioingizwa utasababisha ukweli mzuri kutoka nje. Unaweza kusema jambo sawa kwa "komyuta"- hiyo ni akili yetu. Chochote tunaruhusu katika akili zetu hatimaye kitatoka katika matendo yetu. Yahshua Messiah alifundisha yale yaliyo akilini mwetu na katika mioyo yetu hatimaye yatafichuliwa katika matendo yetu. Kwa hiyo, mawazo mabaya yataongoza kwa matendo ya dhambi. Lakini, ikiwa sheria ya Yahweh imeandikwa mioyoni mwetu, na kuwekwa ndani ya akili zetu, basi utii utatokea. Hii ni sheria kamilifu ambayo imeunganishwa kwa mtu wetu na kwa akili zetu.

Mnyama anaweka alama kwenye mkono wa kuume na kipaji cha uso cha watu wake, kudhibiti mawazo na matendo ya watu wa kidunia. Yahweh anaweka Sheria Yake kwenye kipaji cha uso- katika akili zetu (kumbukumbu, ukumbusho), ambazo hudhubiti mikono yetu ya kuume KUMTII Yeye. Kwa kuongezea, Yahweh anaweka Sheria yake katika akili zetu wakati tunatunza Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu, kama Kutoka 13:9 inavyotuelekeza.***"Ili kwamba sheria ya Yahweh ipate kuwa kinywani mwako."*** Yahweh ametuambia kwamba ***"Mwanadamu haishi kwa MKATE TU, bali huishi kwa KILA litokalo kinywa cha Yahweh."*** (Kumbukumbu la Torati 8:3). Kumbuka kwamba Mkate Usiotiwa Chachu unamaanisha MAFUNDISHO YENYE UZIMA- kutokuwa na unafiki- kuishi kwa yale ambayo Biblia inafundisha.

Katika Kumbukumbu la Torati 11:13, tunapata jambo sawa. ***"Tena itakuwa, MTAKAPOYA-***

***SIKIZA KWA BIDII maagizo yangu, niwaagizayo leo, kwa KUMPENDA Yahweh, Elohim wenu, na KUMTUMIKIA kwa MIOYO YENU YOTE na NAFSI zenu zote, ndipo nitakapowapa mvua ya nchi yenu kwa wakati wake, mvua ya masika, na mvua ya vuli, upate kuvuna nafaka yako, na divai yako, na mafuta yako. Nami nitakupa nyasi katika mashamba yako kulisha wanyama wako wa mifugo, nawe utakula na kushiba. Jitunzeni nafsi zenu, mioyo yenu isije IKADANGANYWA, na MGEUKE KANDO, na kutumikia elohim zingine na kuziabudu; HASIRA ya Yahweh zikawaka juu yenu, naye akafunga mbingu kusiwe na mvua, wala nchi isitoe matunda yake; MKAANGAMIA KWA UPESI mtoke katika nchi nzuri awapayo Yahweh."*** (Kumbukumbu la Torati 11:13-17).

Tii amri, na Yahweh atakubariki. Atawanyeshea mvua kwa wakati Wake, na mtabarikiwa kwa kuzaa matunda. Ukigeuka kando, hata hivyo, na kutumikia elohim wengine, Yahweh ataondoa baraka Zake kutoka kwako na badala yake kukulaaani.***"Jitunzeni nafsi zenu, mioyo yenu isije IKADANGANYWA, na mgeuke kando na kutumikia elohim zingine na kuziabudu*** [kuna mwenye-nguvu wa Kweli mmoja, na Jina Lake ni Yahweh];***hasira ya Yahweh zikawaka juu yenu, naye akafunga mbingu kusiwe na mvua,*** [hakuna Roho Mtakatifu kwako, kutafsiri hili kiroho], ***wala nchi isitoe matunda yake***" Hautakua kiroho, na hatimaye utaangamia.

***"Kwa hiyo yaekeni maneno yangu mioyoni mwenu na rohoni mwenu; yafungeni yawe DALILI juu ya mikono yenu, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yenu."*** (Kumbukumbu la Torati 11:18). Liweke Neno la Yahweh moyoni mwako na katika nafsi yako. Yafunge yawe dalili mkononi mwako. Ruhusu neno la Yahweh kukudhibiti wewe na kila nyanja ya maisha yako- jinsi unavyopata riziki yako na jinsi unavyojiendesha mwenyewe katika uhusiano na binadamu mwenzako. ***"Yatakuwa kama utepe katikati ya macho yenu,"*** haimaanishi filakteria, lakini, badala yake, kama WAISRAELI WA KIROHO, kuwa nazo akilini mwetu na katika kumbukumbu zetu. Ni muhimu kwamba pia tuyafunze kwa watoto wetu, kuwaelekeza kutunza Sheria za Yahweh, pamoja na Amri kumi na Sheria na hukumu zinazoandamana nazo. Ikiwa tutaziandika juu ya miimo ya nyumba zetu za kiroho, tutaondoa ponografia, matumizi ya dawa za kulevya, na muziki wa kilimwengu wenye jeuri potovu ambao unawaelekeza wengi kwenye uasherati. Ikiwa tungefanya hili- kuandika Sheria za Yahweh kwenye malango ya hema zetu za kiroho- tutaondoa dhambi hizo kutoka akilini mwetu na mtindo wa maisha.

Yahweh anaahidi kwamba siku zetu duniani zitaongezeka, vilevile siku za watoto wetu pia. Kama utatembea Njia ya Maisha ya Ufalme sasa, unaweza kuzoea onja ya Ufalme wa Yahweh unaokuja. Utawala wa milenia wa Yahshua duniani humu uko karibu! Je, hilo si jambo la kushangaza? Yahweh ametuahidi mambo haya. Elewa Alama ya Mnyama katika maana ya kiroho, kama tulivyoambiwa kufanya katika Maandiko haya.

**Alama ya Sabato**

Kuna watu wengi duniani leo- Wakr-sto, kwa mfano- wanaodhihaki utunzaji wa Sabato ya siku ya saba. Kuna Wakr-sto wanaodhihaki utunzaji wa siku za sikukuu za Yahweh. "*Unamaanisha nini, lazima tushike sikukuu hizo za zamani za Wayahudi? Hatuadhimishi sikukuu ya Wayahudi,"* lakini tunaadhimisha SIKUKUU ZA YAHWEH. Sabato ya kila wiki, katika siku ya saba ya kila wiki, ni siku ya sikukuu ya **kila juma**. Kwa kuongezea kwa Sabato ya siku ya saba, kuna siku saba za sikukuu za **kila mwaka** vilevile, zilizogawanywa katika misimu mitatu takatifu, ambayo Yahweh ameainisha katika Neno lake. Lazima tutunze siku za Sikukuu ZOTE za Yahweh. ***"Kisha Yahweh akanena na Musa, na kumwambia, Nena na wana wa Israeli, na kuwaambia, SIKUKUU ZILIZOWEKWA za Yahweh, ambazo mtazipigia mbiu kuwa ni MAKUSANYIKO MATAKATIFU; hizi ni sikukuu zangu. Mtafanya kazi siku sita, lakini siku ya saba ni SABATO ya kustarehe kabisa, kusanyiko takatifu, msifanye kazi ya namna yoyote; ni SABATO kwa Yahweh katika makao yenu yote. Sikukuu za Yahweh ni hizi, ni makusanyiko matakatifu, ambayo MTAYAPIGIA MBIU kwa nyakati zake ZILIZOTEULIA."*** (Walawi 23:1-4).

Katika Kutoka 31:13, Yahweh aliamuru Musa ***"Kisha nena na wana wa Israeli, na kuwaambia, hakika MTAZISHIKA sabato zangu, kwa kuwa ni ISHARA…."*** Tena tunaona neno *ishara*. Neno *ishara* lina uhusiano gani hasa kwa alama ya Mnyama, au kuwa na Alama ya Yahweh? Neno *ishara* #226, katika **Strong's Exhaustive Concordance**, ni neno *'oth*, na linamaanisha *ishara, bendera, mnara, ishara, ushahidi*. Ni neno sawa ambalo linatumika katika Mwanzo 1:14, ambapo linasema mianga iliyo mbinguni itakuwa kwa *ishara*-USHAHIDI wa ratiba ya Yahweh ya majira, siku, na miaka. **The Holliday Hebrew Lexicon** inafafanua neno *'oth*, katika uhusiano kwa

Maandiko tunayozingatia, kama *alama ya kutofautisha*.

Kutoka kwa vifungu hivi viwili, Kumbukumbu la Torati 6:8 na Kumbukumbu la Torati 11:18, ambapo neno *ishara* linaonekana, neno la Kiebrania *'oth* linamaanisha **alama ya kutofautisha**. Tunapoiangalia katika suala hili, basi tuchunguze pia Kutoka 31:13, ***"Kisha nena na wana wa Israeli, na kuwaambia, hakika mtazishika SABATO zangu, kwa kuwa ni ISHARA*** [ishara, bendera, *beacon*, ishara, au USHAHIDI]***KATI YA MIMI NA vizazi vyenu vyote, ili mpate kujua ya kuwa MIMI NDIMI YAHWEH NIWATAKASAYE NINYI."*** Hili linahusiana moja kwa moja nyuma kwa Walawi 23, ambapo tunaambiwa kwamba lazima tuadhimishe SABATO (wingi). Sabato ya KILA JUMA (siku ya saba ya wiki) na siku takatifu ZA KILA MWAKA zote zinapangwa katika kifungu KIMOJA. Lazima tutunze kila moja ya Sabato za Yahweh, ili tujue kwamba Yahweh ametutenga KWA KUSUDI TAKATIFU. Neno *kutakaswa* ni *Mekaddishkem*, ambalo linamaanisha **kutengwa au kutakaswa**- kwa KUSUDI TAKATIFU.

Ni **ishara** [alama ya kutofautisha] ***kati YANGU NA NINYI katika vizazi vyenu vyote,"***Yahweh anasema. Yahweh anaendelea***, "Basi MTAISHIKA hiyo sabato*** [siku ya saba ya wiki]***; kwa kuwa ni TAKATIFU KWENU." (Kutoka 31:14).***Ni siku muhimu sana- pengine siku MUHIMU ZAIDI- ya sabato Zake ambazo tunaadhimisha, kwa sababu tunaitunza KILA wiki kwa HESHIMA YA PEKEE kwa Yahweh, kumbukumbu ya UUMBAJI.

Kwa kushika Sabato, tunaonyesha kwamba Yahweh ni Mwenye-nguvu wetu (Elohim), ambaye aliumba mbingu na nchi. Kama alikuwa na nguvu ya kutosha kuumba mbingu na nchi, basi tunapaswa kujisalimisha kwa UTAWALA Wake. Alikuwa na nguvu ya kutosha kutuumba. Alikuwa na mawazo ya kutosha na nguvu kutuumba KWA MFANO WAKE. Kwa hiyo, tunatii Sabato katika heshima kwa amri Zake.

***"Basi MTAISHIKA hiyo sabato; kwa kuwa ni takatifu kwenu; kila mtu ATAKAYEITIA UNAJISI hakika yake atauawa; kwa kuwa kila mtu afanyaye kazi katika siku hiyo, nafsi hiyo ITAKATALIWA MBALI na watu wake."*** (Kutoka 31:14). Kama tu Waisraeli, ambao waliuawa kwa kutotii Sabato katika Kutoka 16 na Hesabu 15, ***kwa kuwa kila mtu afanyaye KAZI katika siku hiyo, NAFSI hiyo ITAKATALIWA MBALI na watu wake***. Ni ya kuvutia kuona uhusiano kati ya moja ya maneno kwa *kazi*, ambalo ni *abad* katika Kiebrania, pia ni neno sawa lililotumiwa kwa kutumikia wenye nguvu wa upagani (Kumbukumbu la Torati 7:16). Yahweh anasema, "Nina watumishi wangu, waabudu wangu, Obadiah wangu." Hii ndiyo sababu tunapata umuhimu mkubwa katika jina **Obadiah School of the Bible**, kwa sababu tunapata umuhimu mkubwa katika jina Obadiah. Lakini watumishi wanaojihudumia wenyewe na kukiuka Sheria za Yahweh, ambao pia WANAFANYA KAZI katika Sabato, pia ni waabudu wa wenye nguvu wa upagani. Je, unaona maana maradufu hapa ambayo inaweza kupatikana na kufikiwa kutoka kwa ufahamu huu? **Wale wanaotumikia wenye nguvu wa upagani wanafaya kazi Sabato,** lakini waabudu wa Yahweh na watumishi wake WANAPUMZIKA katika siku ya kupumzika ambayo ameifanya amri- ambayo aliumba kwa wema wetu.

Hoja hii inasisitizwa mara kadhaa katika Kutoka 31:15-17. ***"Kazi itafanywa siku sita lakini siku ya saba ni Sabato ya KUSTAREHE KABISA, takatifu kwa Yahweh; kila mtu atakayefanya KAZI YOYOTE katika siku ya Sabato, hakika yake ATAUAWA.Kwa ajili ya hayo wana wa Israeli WATAISHIKA Sabato, KUANGALIA sana hiyo Sabato katika vizazi vyao vyote, ni agano la milele. Ni ISHARA kati ya mimi na wana wa Israeli milele...."*** Sabato ni alama ya kutambulisha juu ya Watu wa Yahweh- Waabudu wa Kweli. Katika Ezekieli 8 na Ezekieli 20:12-20, neno sawa, *'oth* linatumika kuhusiana na Sabato (wingi). Yahweh amesema, ***"Nilitoa Sabato yangu kuwa ishara."*** Zote sabato ya kila juma, vilevile siku takatifu za kila mwaka, zimeunganishwa pamoja katika kundi moja hapa.

**Alama juu ya Wale Wanaoungua na Kulia**

Katika Ezekieli 8, tunapata watu wasiotii Yahweh na kufanya machukizo kwa Yahweh. Ninataka kusisitiza, hasa hapa, kwamba wakati Ezekieli anachimba kwenye ukuta na kupata mlango, anapopitia kwa mlango, ni Sanhedrin wa Israeli aliowaona wakifanya machukizo. ***"Na watu sabini wa wazee wa Israeli walikuwa wamesimama na kuzielekea, na katikati yao alisimama Yaazania, mwana wa Shafani; kila mmoja ana chetezo mkononi mwake, na harufu ya moshi wa uvumba ilipaa juu. Kisha akaniambia, mwanadamu, umeyaona wanayotenda wazee wa nyumba ya Israeli gizani, KILA MMOJA NDANI YA VYUMBA VYAKE VYA SANAMU? Maana husema, Yahweh hatuoni, Yahweh ameiacha nchi."*** (Ezekieli 8:11-12).

Vipi kuhusu wewe? Je, unam-




wabudu Yahweh kwa nje, lakini ukimtumikia mwenye nguvu TOFAUTI moyoni mwako? Unaabudu sanamu kwa ndani katika mawazo yako? Ni nini unaficha kutoka kwa ndugu wenzako na dada? Je, **moyo** wako na **akili** ni SAFI mbele za Yahweh, ukimtumikia kwa bidii. Hilo ni swali wewe pekee unaweza kujibu. Yahweh anaona nini iliyo moyoni mwetu. Watu hawa hawakuamini kwamba Yahweh alikuwa Mwenye-nguvu wa Kweli, Aliye na nguvu ya kutosha kuangalia akilini mwao. Yahweh anajua mawazo yetu hasa na nia ya mioyo yetu. Yahweh anajua ni dhambi gani tunayofanya, hata kama tunaficha yale tunafanya kutoka kwa wengine wote. Waisraeli katika Ezekieli 8 walipaswa kuwa watiifu kwa sheria ya Yahweh, ila wanaelezewa kama WASIOTII amri za Yahweh, wakiwa na MACHUKIZO mioyoni mwao.

***"Kisha akalia kwa sauti kuu masikioni mwangu, akisema, waamuru wale wanaousimamia mji wakaribie, kila mmoja na kitu chake cha kuangamiza*** [upanga] ***mkononi mwake*. *Na tazama, watu sita wakaja, wakitokea kwa njia ya lango la juu, lielekeao upande wa kaskazini, kila mmoja ana kitu chake cha kufisha mkononi mwake, na mtu mmoja kati yao amevaa bafta, naye ana kidau cha wino cha mwandishi kiunoni…."*** (Ezekieli 9:1-2).

Cha kuvutia, mtu wa saba, alikuwa na kidau cha wino cha mwandishi, wakati wa sita alikuwa na upanga, silaha ya kuangamiza. Watu sita wa kuchinja na mmoja, wa saba, ataweza kuwa na kidau cha wino cha mwandishi. ***"Na huo utukufu wa Elohim wa Israeli ulikuwa umepanda juu kutoka kwa kerubi, ambaye ulikuwa juu yake, mpaka kizingiti cha nyumba, akamwita mtu yule aliyekuwa amevaa bafta, mwenye kidau cha wino cha mwandishi kiunoni. Yahweh akamwambia, pita kati ya mji, kati ya Yerusalemu, UKATIE ALAMA KATIKA VIPAJI VYA NYUSO vya watu wanaoungua na kulia kwa sababu ya MACHUKIZO yote yanayofanyika kati yake."*** (Ezekieli 9:3-4).

Vipi kuhusu wewe? Je, umejitoa kwa Yahweh na njia Yake ya maisha? Unapozungumza na wale ambao hawajui **njia ya kweli** kwa uzima wa milele, unaweza kuwasahihisha kwa upendo? Je, Neno la Yahweh liko **moyoni** mwako na **akilini** mwako, ili kwamba, unapomwona mtu **akivuka mipaka** ya Sheria ya Yahweh, kwamba amri za Yahweh mara moja zinakuja akilini mwako? Unaweza kunukuu Maandishi hayo? Tunatakiwa kuwa mashahidi wa Yahweh dhidi ya ufisadi wa dunia, dhidi ya mwelekeo uliochukuliwa na dunia.

Katika Ezekieli 9:4, neno *alama* ni *taw*, # 8420 katika

**Strong's Exhaustive Concordance**, na linaandikwa *taw waw*. Linamaanisha, *alama au sahihi*. Kama tunavyoijua, *taw* ni jina la herufi ya mwisho ya alfabeti za Kiebrania, awali likiandikwa kama X. Ni vipi unaandika sahihi yako mwenyewe kama huwezi andika jina lako katika hati? Unaweka X chini. Hati ambazo unaweza kuulizwa kuweka sahihi, zina X katika mstari wa sahihi, mahali unaweka sahihi jina lako, na hivyo, inasimamia sahihi yako. Hapa ndipo unaweka alama yako, hiyo ni, sahihi yako. **Holladay Hebrew Lexicon** pia inasema kwamba inathibitisha hati. Pia inathibitisha **agano**.

Wale wanaojaribu kuishi maisha ya haki wanatiwa sahihi. Hebu tuone ni nini hasa sahihi hiyo. Katika Assemblies of Yahweh, tunafahamiana sana na Ufunuo 14:1, ambayo inavutia sana. Pengine imefanya hisia sawa vilevile. ***"Kisha nikaona, na tazama, huyo mwana-kondoo amesimama juu ya mlima Sayuni, na watu mia na arobaini na nne elfu pamoja naye, WENYE JINA LAKE NA JINA LA BABA YAKE limeandikwa katika vipaji vya nyuso zao."*** Maandiko yanasema akiwa na Jina Lake na Jina la Baba Yake limeandikwa kwenye vipaji vya nyuso zao. Hii ni sahihi ambayo inaandikwa akili mwako, na moyo wako, na iliyopandikwa kwa paji la uso wako. Je, ni kitu kinachoonekana? Hapana, ni SAHIHI ISIYOONEKANA ambayo wewe pekee na Yahweh mnajua iko hapo katika paji la uso wako- akilini mwako.

Zaidi, 2 Timotheo 2:19 inatuambia kwamba 144,000 wanatiwa muhuri wa Jina la Baba na Mwana. ***"Lakini, msingi wa Yahweh ulio imara umesimama, wenye MUHURI huu, Yahweh awajua walio wake. Na tena, KILA ALITAJAYE JINA LA YAHWEH NA AUACHE UOVU."*** Ikiwa unatumia majina ya Yahweh na Yahshua aliye Messiah, basi ni muhimu kwako KUACHANA NA UVUNJAJI WA SHERIA, au Yahweh **ataihitaji kutoka kwako hatimaye.** Hii ni Alama ya Yahweh- sahihi ya Yahweh juu ya akili yetu- muhuri wake wa idhini ambao anaweka juu yetu. SNB


# Commentary on the Book of Revelation Volume Two

# THE MARK OF THE BEAST

Juzuu ya pili ya mfululizo wa **Commentary on the Book of Revelation** sasa inapatikana kwa usambazaji. Juzuu la pili lina kurasa 90 za utafiti bora wa kusoma Biblia.


Ili kupata habari zaidi jinsi unaweza nunua nakala ya kitabu hiki, tafadhali andika kwa:

**ASSEMBLIES OF YAHWEH**
PO Box C • Bethel, PA 19507
(717) 933-4518

**Also available for online purchase at www.assembliesofyahweh.com**



# Taking Yahweh's Truth with you wherever you go




- Wealth of scholarly resources at your fingertips
- Complete library of available literature
- Sermons available 24/7
- Comprehensive catalog of **The Sacred Name Broadcaster**
- Truth–From Genesis to Revelation, heralded to all the world!

**Download the new Assemblies of Yahweh app available in Apple or Android platforms**

Download on the App Store

GET IT ON Google Play


# *Zawadi yetu kwa Ulimwengu*

## Maarifa ya Neno la Uzima

*Continued from page 9.*

tumaini kwamba utaiona kuwa zawadi yetu ya ujuzi kwako. Ingawa watu wamekuwa kwenye orodha ya barua ya **The Sacred Name Broadcaster** kwa miaka mingi, wengine hawajawahi kuchangia. Hata hiyvo, wameweza kuongeza ujuzi wao wa kibinafsi wa Biblia na Neno la Yahweh, na tunashukuru kwa hilo.

Hii ni zawadi yetu kwa ulimwengu, ili kwamba wote ambao ni wenye dhati na wana hamu kuokolewa wanaweza kupokea maarifa ya Neno la uzima.

Kujitolea kwetu kwa ajili ya watu wa ulimwengu kunamaanisha kwamba tunampenda kila mtu ambaye anajitahidi kuishi kwa ajili ya Aliye Juu Zaidi.

Tunakupenda pia. Hii ndiyo ishara ya ibada ya kweli. ***"Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane hivyo. Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi."*** (Yohana 13:34-35). SNB

**Tafadhali hakikisha kuwa umepitia logi ya redio na televisheni kwenye kurasa zifuatazo ili kubaini kama unaweza kusikiliza kwa The Sacred Name Broadcast na The Sacred Name Telecast kwenye vituo mbalimbali katika mtandao wetu wa kibiashara**

# THE SACRED NAME PROGRAMS

## TELEVISION

*These television stations air **The Sacred Name Telecast**.*
*Check the program time and frequency of the station in your area.*

**WDVB New York City, NY**
Channel 23.3 and
Verizon FIOS Channel 477
Sunday 9:30 AM

**WMDE Washington D.C.**
Channel 36
Sunday 7:30 AM ET

**WRCX Dayton, OH**
Channel 40.1 and
Time Warner Channel 22
Sunday 9:30 AM

**WZXZ Orlando, FL**
Channel 36.1
Sunday 9:30 AM

**WJDE Nashville, TN**
Channel 31.4
Sunday 8:30 AM

**WLOO Jackson, MS**
Channel 35.2 and
Comcast Channel 220
Sunday 8:30 AM

**WKYK Little Rock, AR**
Channel 30.3
Sunday 8:30 AM

**WLFT Baton Rouge, LA**
Channel 30.4
Sunday 8:30 AM

**KUMY Beaumont, TX**
Channel 22.1
Sunday 8:30 AM

**KHLM Houston, TX**
Channel 43.3

Sunday 8:30 AM

**KXLA Los Angeles, CA**
**Channel 44.1**
Sunday 9:00 - 9:30 AM

## RETRO TV

***Sunday 7:30 AM Eastern Time***

**CONNECTICUT**
HARTFORD / NEW HAVEN
WETN-LD • Channel 16.1

**FLORIDA**
GAINESVILLE
WGVT-LD • Channel 26.1

JACKSONVILLE
WJVF-LD • Channel 23.2

ST. AUGUSTINE
WQXT-CD • Channel 12.4

MOBILE / PENSACOLA (FT WALTON BEACH)
WBQP-CD • Channel 12.4

ORLANDO / DAYTONA BEACH / MELBOURNE
WZXZ-CD • Channel 36.1

TAMPA / ST. PETE (SARATOSA)
WDNP-LD • Channel 36.2

WEST PALM BEACH / FT. PIERCE
Palm Bay, Sebastian, Vero Beach, Port St. Lucie
WMMF-LD • Channel 19.12

**GEORGIA**
ATLANTA
WDNV-LD • Channel 12.5

GAINESVILLE
WGVT-LD • Channel 26.1

CHATTANOOGA / Dalton
WDNN-CD • Channel 49.3
OptiLink Ch. 142,
VIDLink Ch. 27

COLUMBUS, GA (OPELIKA, AL)
WXVK-LD • Channel 30.2

SAVANNAH
W31FE-D • Channel 23.2

**KENTUCKY**
RICHMOND
WBON-TV9 • Channel 9.5

LOUISVILLE
WBNM-LD • Channel 50.9

**MASSACHUSETTS**
BOSTON (MANCHESTER)
WWDP • Channel 46.5

BURLINGTON / PLATTSBURGH
Winchendon
WVMA-CD • Channel 17.2

**MICHIGAN**
DETROIT
WHPS-CD • Channel 15.4

GRAND RAPIDS / KALAMAZOO
BATTLECREEK
WLLA • Channel 64.5

**NEW YORK**
ALBANY / SCHENECTADY / TROY
WYBN-LD • Channel 14.4

Mid Hudson Cable Ch. 147

BUFFALO
WBNF-CD • Channel 15.4

ROCHESTER, NY
WGBT-CD • Channel 46.2

**NORTH CAROLINA**
GREENVILLE / NEW BERN / WASHINGTON
WJGC-LD • 33.2

GREENVILLE / SPARTANBURG / ASHEVILLE / ANDERSON
WASV-LP • Channel 50.2

RALEIGH / DURHAM (FAYETTEVILLE)
WDRH-LD • Channel 16.2

**OHIO**
CLEVELAND / AKRON (CANTON)
Canton, Alliance
WIVM-LD • Channel 39.5

New Philadelphia
WIVD-LD • Channel 26.5

MCTV Cable Canton, OH • Digital Ch. 129

New Philadelphia
WIVN-LD • Channel 29.5

COLUMBUS
WOOH-LD • Channel 29.2

**PENNSYLVANIA**
PHILADELPHIA
WDPN-TV • Channel 2.5

RCN ALLENTOWN Ch. 27 / Philadelphia Ch. 25
Service Electric Ch. 108 /
Verizon FiOS Ch. 480

PITTSBURGH
WPTG-CD • Channel 69.3

WILKES BARRE-SCRANTON-HAZELTON
WSRG-LD • Channel 59.2

Wilkes-Barre, Scranton
WRLD-LD • Channel 30.10

**SOUTH CAROLINA**
CHARLESTON, SC
WLOW-LD • Channel 19.2

GREENVILLE / SPARTANBURG / ASHEVILLE / ANDERSON
WNGS-LD • Channel 50.2

**TENNESSEE**
CHATTANOOGA
WOOT-LD • Channel 6.2

KNOXVILLE
WKXT-LD • Channel 34.2

Charter Ch. 8, Spectrum Ch. 20

**WASHINGTON, D.C.**
WASHINGTON, DC (HAGERSTOWN)
Baltimore / Annapolis / Dover
WMDE • Channel 36.4

***Sunday 6:30 AM Central Time***

**ALABAMA**
BIRMINGHAM (ANNISTON AND TUSCALOOSA)
WSWH-LD • Channel 46.2

COLUMBUS, GA (OPELIKA, AL)
Auburn
WQMK-LD • Channel 18.1
DOTHAN
WJJN-LD • Channel 20.4

HUNTSVILLE / DECATUR (FLORENCE)
WNAL-LD • Channel 27.2

MONTGOMERY / SELMA
WAAO-LD • Channel 40.1

Andy Cable Ch. 14, Ch. 79.2

**ARKANSAS**
SHREVEPORT / Texarkana
KLFI-CD • Channel 35.6

**ILLINOIS**
PEORIA / BLOOMINGTON
WSIO-LD • Channel 51.2

**INDIANA**
EVANSVILLE
WYYW-CD • Channel 15.2

INDIANAPOLIS
WSWY-LD • Channel 21.2

**IOWA**
DES MOINES / AMES
WBXF-CD • Channel 28.5

**KANSAS**
KANSAS CITY
Kansas City - Leavenworth - Lawrence - Olathe
KCKS-LD • Channel 25.8

TOPEKA
WROB-LD • Channel 25.8

WITCHITA / HUTCHINSON PLUS
KSMI-LP • Channel 30.2

AT&T U-Verse Ch. 51
USA Connections Ch. 451

**LOUISIANA**
BATON ROUGE
WRUG-LD • Channel 50.2
LAFAYETTE, Lake Charles
K21OB-D • Channel 21.2

SHREVEPORT
KVPO-LD • Channel 30.2

Texarkana
KLFI-CD • Channel 35.6

**MINNESOTA**
MINNEAPOLIS / ST. PAUL
KKTW-LD • Channel 19.2

ALEXANDRIA
K16CO-D • Channel 16.1

**MISSOURI**
JOPLIN-PITTSBURG
KJLN-LD • Channel 50.2

SPRINGFIELD, MO
KSFZ-LD • Channel 41.2

ST. LOUIS
KUMO-LD • Channel 51.3
WPXS • Channel 13.2

**OKLAHOMA**
OKLAHOMA CITY
KWRW-LD • Channel 33.2

TULSA
KTUO-LD • Channel 22.2

**SOUTH DAKOTA**
RAPID CITY
KRPC-LP • Channel 33.2

SIOUX FALLS (MITCHELL)
KCPO-LP • Channel 26.2

**TENNESSEE**
NASHVILLE
WWHL-LD • Channel 27.2

Dickson
WDHC-LD • Channel 11.1

UNION CITY/PADUCAH / CAPE GIARDEAU / HARRISBURG

WUWT-CD • Channel 26.1

Charter Ch. 8, Spectrum Ch. 20

**TEXAS**
BEAUMONT-PORT ARTHUR
KAOB-LD • Channel 27.2

CORPUS CHRISTI
K33QP-D • 33.2

DALLAS / FT. WORTH
KFWD • Channel 52.4

HOUSTON
KVQT-LD • Channel 21.2

SAN ANTONIO
KRTX-LP • Channel 20.2

TYLER-LONGVIEW (LUFKIN & NACOGDOCHES)
KLNM-LD • Channel 42.4

WACO / TEMPLE / BRYAN
Bryan, College Station
K20KJ-D • 20.2

**WISCONSIN**
MILWAUKEE
WTAS-LD • Channel 23.6

***Sunday 8:30 AM Mountain Time***

**ARIZONA**
PHOENIX (PRESCOTT)
Phoenix
KFPB-LD • Channel 31.4

**COLORADO**
DENVER / Boulder
KAVC-LD • Channel 48.2

**MONTANA**
BILLINGS / Hardin
KQHD-LD • Channel 43.1

BUTTE / BOZEMAN
Townsend
K04QX-D • Channel 8.1

**NEW MEXICO**
ALBUQUERQUE-SANTA FE
KCHF • Channel 11.7

**UTAH**
SALT LAKE CITY
Manti, Ephram
KMTI-LD • Channel 8.1

Manti Telephone Ch. 22, South / Central Telephone Ch. 23

PIUTE, RICHFIELD
KSVC-LD • Channel 8.1

***Sunday 7:30 AM Pacific Time***

**CALIFORNIA**
CHICO / REDDING
KXCH-LD • Channel 19.2

FRESNO / VISALIA
KJKZ-LD • Channel 27.4

LOS ANGELES
KBEH • 63.3

VICTORVILLE
KVVB-LP • Channel 33.3

Cox (Orange County) Ch. 817 / Spectrum Ch. 1293 / Frontier Fios Pomona Ch. 469

SACRAMENTO / STOCKTON / MODESTO
Sacramento / Elk Grove
KSTV-LD • Channel 32.2

SAN DIEGO
KSDY-LD • 50.3

SAN FRANCISCO / OAKLAND / SAN JOSE
KQSL-LD • Channel 17.11

Santa Rosa
KUKR-LD • Channel 27.11

**NEVADA**
LAS VEGAS
KVGA-LD • Channel 51.2

RENO
KCNL-LD • Channel 3.7

**OREGON**
EUGENE
Cottage Grove
K30OC-D • Channel 44.8

PORTLAND
KJYY-LD • Channel 29.5

SALEM
KJWY-LD • Channel 21.5

YAKIMA / PASCO / RICHLAND / KENNEWICK
Milton Freewater
K20MJ-D • Channel 40.1

**WASHINGTON**
SEATTLE / TACOMA
KYMU-LD • Channel 6.4

## Cable and Satellite

**Cars.TV**
AT&T U-verse, Channels 280 & 1280
Verizon FiOS Channel 599
Sunday 7:00-7:30 AM ET

**Comedy.TV**
AT&T U-verse, Channels 281 & 1281
Verizon FiOS Channel 695
DirecTV Channel 382
Sunday 7:00-7:30 AM ET

**ES.TV**
AT&T U-verse, Channels 282 & 1282
Verizon FiOS Channel 558
Sunday 7:00-7:30 AM ET

**JusticeCentral.TV**
AT&T U-verse, Channels 166 & 1166
Verizon FiOS Channel 186
DirecTV Channel 383
Dish Network Channel 240
Sunday 7:00-7:30 AM ET

**MyDestination.TV**
AT&T U-verse, Channels 284 & 1284
Verizon FiOS Channel 674
Sunday 7:00-7:30 AM ET

**Pets.TV**
AT&T U-verse, Channels 279 & 1279
Verizon FiOS Channel 633
Sunday 7:00-7:30 AM ET

**Recipe.TV**
AT&T U-verse, Channels 283 & 1283
Verizon FiOS Channel 676
Sunday 7:00-7:30 AM ET

**Chicago/Upper Midwest**
Comcast Cable Channel 138-TLN
Streaming @ www.tln.com
Tuesday 10:30 - 11:00 PM CT
Thursday 11:00-11:30 AM CT

***Canada***

**CTV-CIVT**
Channel 32, and
cable 8 and 9 Vancouver, British Colombia
Sunday 5:00–5:30 AM

**CTV Nationwide on Satellite**
Bell ExpressVu 250,
Shaw Direct (Star Choice) 321
Rogers Cable 112

***Caribbean Region***

**HTS**
Channel 4, St. Lucia
Sunday 10:30–11:00 AM

**Cable TV**
Channel 15, St. Maarten
Sunday 3:30–4:00 PM

**MSR Cable TV**
Channel 6, St. Martin
Sunday 10:00–10:30 AM, 7:00–7:30 PM

***Please be sure to check local listings.***

**Sirius/XM**
**Channel 131**
**Sunday**
**9:30 PM ET**



# RADIO

*Check the time and frequency in your area.*

## Atlantic

***West Indies***

**DBS Radio (Dominica)**
88.1 FM
Sunday 9:00–9:30 AM

**WeeFM Radio (Grenada)**
93.3
Sunday 8:30–9:00 AM

**Guyana Radio Roraima**
760
Sunday 6:00–6:15 AM

**Radio St. Lucia** 660
Sunday 6:00–6:30 AM

**Radio PJD2 (St. Maarten)**
1300
Sunday 5:30–6:00 AM

**Trinidad Radio Power**
102.5
Sunday 6:45–7:00 AM

## Eastern

***Pennsylvania***

**WWSM** (wwsm.us), Lebanon
Sunday 7:30–8:00 AM

***West Virginia***

***WWVA** 1170, Wheeling
Friday 10:00–10:30 PM (also streamed)

***Ohio***

***WCKY** 1530, Cincinnati
Sunday 6:30–7:00 AM

## Central

***Texas***

***KCKM** 1330 AM, 98.7 FM, Odessa
Sunday 8:00—8:30 AM

***Tennessee***

***WSM** 650 AM Nashville
Sunday 5:30–6:00 AM

## Western

***California***

***KDIA** 1640 AM, San Francisco Bay Area
Sunday 6:00—6:30 AM

## Nigeria

**Bayelsa State Radio** 97.1 FM
**Rivers States Ray Power Radio** 105.5 FM
**Abia State Radio** 88.1 FM
**Benue State Radio** 95.0 FM
**Rock City Radio** 101.9 FM
**Invicta Radio, Kaduna** 98.9 FM

****Indicates a powerful station heard over wide area***

*Sacred Name Broadcaster*
*Bethel, PA 19507*

PERIODICAL
Reading, PA

# The Sacred Scriptures, *Bethel Edition*




***"Uwatakase kwa ile kweli; neno lake ndiyo kweli."***

(JOHN 17:17)

*Neno safi la Ukweli la Yahweh lina uwezo wa kukata kupitia upotoshaji na kuweka mambo katika mtazamo wake unaofaa.*

*The Sacred Scriptures, Bethel Edition, inapatikana katika matoleo ya ngozi, na ya jalada ngumu.*

*Ili kupata nakala yako ya tafsiri hii bora, andika kwa maelezo ya sasa ya bei. Au upige (717) 933-4518*

**Sasa inapatikana kwenye Kindle**

www.assembliesofyahweh.com